**BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA UCHUMI KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAAGIZO YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022 KWA AFISI YA RAIS KAZI UCHUMI NA UWEKEZAJI.

**Mheshimiwa Spika,**

Awali ya yote, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu, Mwingi wa Rehema ambaye ametujaalia uzima na afya njema na kutuwezesha kukutana leo hii tukiwa ndani ya Baraza lako tukufu, tukiendelea na utekelezaji wa majukumu yetu mbali mbali ya kuwatumikia wananchi wetu.

**Mheshimiwa Spika,**

Pongezi za dhati tunazitoa kwako Mheshimiwa Spika pamoja na wasaidizi wako, Mheshimiwa Naibu Spika na Wenyaviti wa Baraza kwa jinsi mnavyoliendesha Baraza hili tukufu kwa busara, hekima na umahiri mkubwa.

**Mheshimiwa Spika,**

Nichukue fursa hii kwa niaba ya Kamati ya Uchumi kumpongeza kwa dhati kabisa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi kwa uongozi wake wa busara uliojaa hekima. Namuomba Mola mtukufu amzidishie afya njema na maisha marefu ili tuzidi kunufaika na uongozi wake. Aidha, tunatoa pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Othman Masoud Othman, Makamu wa Kwanza wa Rais na Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla, Makamu wa Pili wa Rais

kwa msaada mkubwa wanaompatia Mheshimiwa Rais katika kutekeleza majukumu ya kila siku ya uongozi wa nchi hii.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yetu inazishukuru Wizara zote inayozisimamia kwa imani waliyonayo kwetu katika kutekeleza majukumu yetu ya kila siku. Shukurani za pekee ziende kwa Uongozi wa Wizara ya Nchi, Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji kwa mashirikiano wanayotuonesha katika kutekeleza majukumu ya Kamati yetu. Tunawaomba wazidishe mashirikiano hayo ili kwa pamoja tuwatumikie wananchi wa Zanzibar kwa ufanisi mkubwa.

**Mheshimiwa Spika,**

Nichukue fursa hii kumpongeza Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji kwa ushirikiano anaouonesha wakati wote wa kazi za Kamati. Kadhalika, nawapongeza Makatibu Wakuu, Manaibu Katibu Wakuu na Watendaji wote wa Wizara hii kwa namna wanavyotekeleza majukumu yao ya Kitaifa na kuwasilisha kwa wakati taarifa ya utekelezaji wa maagizo ya Kamati yetu pamoja na kutupatia majibu fasaha katika kikao cha majadiliano ya utekelezaji wa maagizo hayo.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa mujibu wa Kanuni ya 107 (3) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi Toleo la 2020 ambayo maelekezo yake yanapatikana kwenye Jadweli la kwanza, Kamati yetu ina jukumu la kuchambua ahadi zote za Wizara zilizo chini yake kama zitakavyokua zikitolewa katika Baraza na Kufuatilia utekelezaji wa ahadi hizo.

Kwa mnasaba huo, Kamati ilikutana na Wizara ya Nchi, Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji tarehe 29/08/2022 na kupokea taarifa ya utekelezaji wa maagizo ya Kamati kwa Wizara hiyo yaliyotokana na Ripoti ya Kamati kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

**Mheshimiwa Spika,**

Nichukue fursa hii kuwashukuru sana Wajumbe wote wa Kamati ya Uchumi ya Baraza la Wawakilishi kwa mashirikiano ya hali ya juu waliyoyaonesha katika kutekeleza majukumu yetu ya Kamati hususani katika kujadili taarifa ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Maagizo ya Kamati kwa Afisi ya Rais Kazi, Uchumi na Uwekezaji kuhusu utekelezaji wa Maagizo ya Kamati yetu. Kwa heshima kubwa naomba kuwatambulisha kwa majina Wajumbe hao kama ifuatavyo:

1. Mhe. Sabiha Filfil Thani - Mwenyekiti
2. Mhe. Dkt. Soud Nahoda - M/Mwenyekiti
3. Mhe. Rukia Omar Ramadhan - Mjumbe
4. Mhe. Hassan Hamad Omar - Mjumbe
5. Mhe. Panya Ali Abdalla - Mjumbe
6. Mhe. Ameir Abdalla Ameir - Mjumbe
7. Ndg. Nouman Thabit Nouman - Katibu
8. Ndg. Asma Ali Kassim - Katibu

**Mheshimiwa Spika,**

Katika utekelezaji wa agizo la kuyafuatilia maeneo waliyokabidhiwa

wawekezaji ambayo kwa muda mrefu hayajaendelezwa, Wizara kupitia ZIPA imechukua hatua mbali mbali lakini pia Kamati inaiomba Serikali kuu kuingilia kati suala hili kwani limekuwa ni tatizo sugu na la muda mrefu.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yetu imearifiwa kuwa ZIPA inakabiliana na changamoto ya upatikanaji wa ardhi eneo la Mazizini ambalo linalengwa kujengwa jengo jipya la ofisi yake. Ujenzi huo ni muhimu katika utekelezaji wa agizo la Kamati la kujenga jengo jipya linalokwenda sambamba na hadhi ya taasisi hiyo kwa uchumi wa nchi yetu. Hivyo, Kamati inaiomba Serikali kupitia Wizara inayohusiana na ardhi kuipatia ZIPA hati ya eneo la ujenzi wa ofisi Mazizini kwa ajili ya kuanza mchakato wa ujenzi ambao tayari sehemu ya gharama zake zimeshapata mfadhili.

**Mheshimiwa Spika,**

Udororaji wa shughuli za uwekezaji nchini unaotokana na mahusiano dhaifu baina ya taasisi za Serikali ni suala lisilokubalika kwa maslahi ya Taifa hili. Pamoja na utekelezwaji wa dhana ya "one stop center", bado Kamati inasisitiza suala la kuwepo kwa Afisa mwenye mamlaka ya kufanya maamuzi katika uhaulishaji wa ardhi kwenye kituo hicho ili tufikie lengo la kuwapatia huduma wawekezaji wenye sifa kwa muda wa masaa 24. Aidha, Kamati inaiomba Wizara husika kulifanyia haraka suala la upimaji wa ardhi jambo ambalo linazorotesha mikakati ya uwekezaji.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inashauri Wizara kupitia ZIPA iwe makini kwenye utoaji wa vibali

vya uwekezaji nchini kwani imebainika kuwa wengi kati ya wawekezaji hao ni wababaishaji na huwa ni madalali wa kuuza maandiko ya miradi hiyo duniani lakini wanapopata fedha hizo huzitumia kwa shughuli zao nyengine na hawarudi kutekeleza miradi iliyokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yetu imearifiwa kuwa suala la uwekezaji katika sekta binafsi nchini linaendelea kusimamiwa na ZIPA. Hata hivyo, imebainika kuwa maafisa Utumishi wa taasisi nyingi za binafsi si Wazanzibari na hivyo huitumia fursa hiyo kuajiri watu wao. Hivyo, tunaiomba Serikali kuwekeza kikamilifu kwenye taaluma ya vijana wetu ili kuondokana na kikwazo cha kutokuwa na sifa za kuongoza katika taasisi hizo.

Aidha, Kamati yetu inaendelea kushauri utekelezaji wa sheria za kazi usimamiwe kikamilifu nchini ili kulinda ajira za vijana wetu kama zilivyo nchi nyengine za visiwa.

**Mheshimiwa Spika,**

Viwanda vya uzalishaji nchini bado vinaendelea na kukumbana na changamoto ya soko la bidhaa zao kutokana na kushindwa kuingiza bidhaa hizo kwenye soko la Tanzania Bara ambako ndiko kwenye soko kubwa. Pamoja na majibu mazuri ya Wizara juu ya suala hili, bado Kamati inaendelea kushauri uandaaji wa mkakati wa sera ya uendelezaji wa viwanda ufanywe kwa haraka na kuendelea kufanya mazungumzo na wenzetu wa Tanzania Bara ili kuwalinda wazalishaji wetu wa ndani kwani kushindwa kuviendeleza viwanda hivyo kunapelekea ukosefu wa ajira kwa vijana wetu.

**Mheshimiwa Spika,**

Katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya uwekezaji nchini, Kamati inaishauri Wizara kuwasiliana na ZAWA kabla ya kuanza kwa miradi hiyo ili kuepusha uvunjaji wa miundombinu kwa ajili ya upitishaji wa miundombinu ya maji. Hii itaiepusha Serikali na kuingia hasara ya kubomoa na kujenga kwenye maeneo hayo hayo.

**Mheshimiwa Spika,**

Uimarishaji wa sekta binafsi nchini ni chachu ya maendeleo. Kwa kulitambua hilo, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaendelea kushirikiana na Sekta binafsi katika miradi mbalimbali ya maendeleo kwa njia ya PPP (Public Private Partnership). Kamati yetu imeridhishwa na mipango ya uimarishaji wa sekta ya umma na sekta binafsi (PPP) ambapo tayari profile ya mradi huo imeshaandaliwa na inatarajiwa kutumika katika miradi mbali mbali ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,**

Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi umeanzishwa chini ya sheria ya Kuanzisha Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Zanzibar ya mwaka 2022 kwa ajili ya kusimamia masuala yote yanayohusiana na uwezeshaji wananchi kiuchumi kwa wajasiriamali na wafanyabiashara ndani ya Zanzibar ili kukuza na kuanzisha fursa za ajira.

Pia Wakala unakusudia kuhakikisha kwamba huduma zote za mikopo, mafunzo, miundo mbinu na masoko kuhusuiana na uwezeshaji wananchi kiuchumi zinapatikana na wajasiriamali na wafanyabiashara kwa lengo la

kushajiisha maendeleo endelevu katika sekta za kiuchumi.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inatoa pongezi kwa Ndugu Juma Burhan Mohammed kwa kuteuliwa kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa wakala huu. Kamati yetu imearifiwa juu ya maendeleo mazuri ya Wakala huu lakini pia unakabiliwa na changamoto mbalimbali. Kwa mnasaba huo, Kamati inashauri Wakala kuondoa urasimu kwa waliokamilisha maombi ya mkopo na kuwapatia fedha au vifaa kwa wakati. Aidha, tunashauri Wakala uondokane na kutekeleza shughuli za muda mfupi bali uwe na mipango endelevu ya kuzalisha ajira kwa vijana wetu.

**Mheshimiwa Spika,**

Mwisho napenda kuwashukuru na kuwapongeza tena viongozi na watendaji wote wa Wizara ya Nchi Afisi ya Rais Kazi, Uchumi na Uwekezaji kwa juhudi wanazozichukua katika kutekeleza kazi zao pamoja na ushirikiano wao kwa Kamati hii.

Aidha, nawashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa kunisikiliza kwa makini wakati wote nilipokuwa nikiwasilisha hotuba hii.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa niaba ya Kamati yangu naomba Kuwasilisha.

Ahsante,



Mhe. Sabiha Filfil Thani,

Mwenyekiti,

Kamati ya Uchumi,

Baraza la Wawakilishi,

**Zanzibar**.